Jarida la Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar

# SHERIA NA HAKI

*Kwa kila Mwananchi*

Ifanye haki
Iwe shauku

Toleo Na. 005 | Jarida la kila miezi mitatu | Januari - Machi, 2011

# Hongera Jarida kutimiza mwaka mmoja

**WASOMAJI** wetu wapenzi tunapenda kuchukua nafasi hii adhimu kukujulisheni kwamba Jarida la "Sheria na Haki" linalochapishwa na Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar (ZLSC) kila miezi mitatu linatimiza mwaka mmoja mwezi wa April 2011.

Jarida liltakuwa na kurasa 20 badala ya 16.

Jarida hili linalosambazwa kila pembe ya Zanzibar na baadhi ya sehemu za Tanzania Bara. Lilianzishwa mwezi April mwaka jana na kuzinduliwa na aliyekuwa Waziri wa Katiba na Utawala Bora Mheshimiwa Ramadhan Abdullah Shaaban ambaye kwa sasa ni Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali.

Uanzishaji wa Jarida hili ni miongoni mwa malengo ya Kituo kwa kutoa elimu ya sheria kwa wananchi wote waliopo mjini na vijijini hususan wasiojiweza na maskini ambao wanahitaji msaada wa sheria.

Sambamba na Jarida hili, Kituo kinaendelea kutoa elimu ya Sheria kupitia televisheni na redio za umma na binafsi, kuandaa semina na makongamano na tafiti mbali mbali za Sheria ambazo husambazwa kwa wananchi ili kuongeza uwezo wao wa sheria.

Wazo la kuanzishwa Jarida lilibuniwa tokea Kituo kilipoanzishwa mwaka 1992 na waasisi wake Marehemu Profesa Haroub Miraji

Inaendelea Uk. 3




Usawa mbele ya sheria Katiba ya Zanzibar na utekelezaji wake Uk. 4

Ijue sheria mikataba ya kazi Zanzibar Uk. 6

Wananchi lazima washirikishwe kutunga Katiba ya nchi yao Uk. 8

Jaji Mkuu mstaafu amaliza mkataba wake Uk. 18

# Watoto watolewa jela

**WATOTO** wawili waliofungwa jela miezi mitatu kila mmoja waliachiliwa huru kufuatia Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar (ZLSC) Pemba, kuingilia kati.

Hakimu wa Mahkama ya Wilaya ya Konde, Bwana Mohammed Amour aliwatia hatiani kwa wizi wa nazi nane 8 na kuwapa adhabu ya kutumikia kifungo cha miezi mitatu katika Chuo cha Mafunzo kiliopo Kangangani, Pemba.

Kabla ya kutolewa jela, watoto hao (majina yanahifadhiwa) walichanganywa na wafungwa watu wazima na walikwishatumikia mwezi mmoja kati ya kifungo cha miezi mitatu.

Inaendelea Uk. 3

Jarida la Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar

Ifanye haki

# SHERIA NA HAKI

*Kwa kila Mwananchi*

Iwe shauku

Toleo Na. 005 | Jarida la kila miezi mitatu | Januari - Machi, 2011

# Wasaidizi wa sheria wafanya mitihani

WASAIDIZI wa Sheria *(paralegals)* wamefanya mitihani wa kumaliza mwaka wa kwanza wa masomo ya sheria yanayotolewa na Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar (ZLSC).

Afisa Mdhamini wa Mafunzo ya Wasaidizi wa Sheria, Mtumwa Sandal, alisema jumla ya wasaidizi wa sheria 61 walifanya mitihani, kati ya hao 36 kutoka Unguja na 25 kutoka Pemba walifanya mitihani.

Alisema wanawake walikuwa 17, kati ya hao 10 kutoka Unguja na saba kutoka Pemba. Aidha, wanaume waliofanya mitihani walikuwa ni 44, kati ya hao 26 kutoka Unguja na 18 kutoka Pemba.

Wasaidizi wa sheria walifanya mitihani ya masomo ya Sheria ya Uhalifu na Mwenendo wa Makosa ya Jinai *(Criminal Law and Criminal Procedure)*, Sheria ya Mikatiba *(Law of Contracts)*, *Legal Method* na *Legal System*.

Kwa mujibu wa Mdhamini wa Mafunzo hayo, wasaidizi wa sheria waliopo katika majimbo yote 50 ya uchaguzi yaliyopo Unguja na Pemba watasoma miaka miwili ili kupata ujuzi wa sheria kwa ajili ya kutoa elimu ya sheria kwa wananchi.

Aidha, mafunzo hayo yanawajumuisha baadhi ya askari polisi na askari kutoka baadhi ya Vikosi vya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

## Haki ya kucheza

Leo nasemea haki,Watoto nawapatiwe
Kucheza wastahiki,Viwanja nawatengewe
Wasiachwe kwenye dhiki, Akili zao zituwe
Haki yao ya kucheza, Watoto wasinyang'anywe

Zao haki ziko nyingi, Mkataba metamka
Usajili ni msingi, Na elimu kadhalika
Wasipewe kazi nyingi, Wapate kupumzika
Haki yao ya kucheza, Watoto wasinyang'anywe.

Kifungu kumi na mbili, Mkataba Afrika
Watoto wastahili, Ustawi kuwafika
Wakisha rudi skuli, Wapate kupumzika
Haki yao ya kucheza, Watoto wasinyang'anywe.

Ila haki ya kucheza, Wakubwa wanaipora!
Viwanja wanaviuza, Kwa wafanya biashara
Wamekosa mwa kucheza, Na kujenga afya bora
Haki yao ya kucheza, Watoto wasinyang'anywe

Watoto wanalaumu, Hakuna wa kusikiza
Tunajitoa fahamu, Mkataba twaubeza
Watoto twawadhulumu, Haki yao ya kucheza
Haki yao ya kucheza, Watoto wasinyang'anywe

Sauti zao ni ndogo, Wakubwa twazipuuza
Kwa amri za vigogo, Maeneo yanauzwa
Watoto mepata pigo, Hawanapo pa kucheza
Haki yao ya kucheza, Watoto wasinyang'anywe

Maeneo yamaliza, Watoto wamashakani
Wanakosa pa kucheza, Wabakia upenuni
Na humo twawafukuza, Waharibu bustani!!
Haki yao ya kucheza, Watoto wasinyang'anywe

Mbona watoto watengwa, Yao haki iko wapi?
Kila eneo lajengwa, Watoto wacheze wapi?
Kwanini wana wavungwa, Viwanja vyao ni vipi?
Haki yao ya kucheza, Watoto wasinyang'anywe

Twaomba miji ipangwe, Usumbufu kuondoa
Na maeneo yatengwe, Watoto kufurahia
Haki zao zisipingwe, Vyema wapate kukua
Haki yao ya kucheza, Watoto wasinyang'anywe.

**SAID RASHID HASSAN**
**ZLSC – PEMBA.**



***Baadhi ya wasaidizi wa Sheria wa ZLSC wakifanya mitihani yao ya sheria kwa mwaka wa mwanzo kisiwani Pemba.***



***Baadhi ya wasaidizi wa Sheria wa ZLSC wakifanya mitihani yao ya sheria kwa mwaka wa mwanzo.***